# Wadau waridhika na usalama wa watalii ila mazingira ya kibiashara yanawatia shaka



Watalii wengi wanaokuja nchini kutoka Bara la Ulaya hupenda kutembelea mbuga za wanyama

**Alawi Masare**, Mwananchi

Kwa muda mrefu, wadau wa sekta ya utalii nchini walikuwa wakipigia kelele kuhusu usalama wa watalii na kutaka mabadiliko katika huduma za kipolisi.

Chama cha Wafanyabiashara za Utalii Tanzania (Tato) kiliwahi kufanya utafiti na kupendekeza kufanyika mabadiliko kadhaa ikiwamo kuundwa kwa vituo maalum vya kuhudumia watalii wa kigeni.

Pendekezo hilo lilipokelewa na Serikali ya Awamu ya Nne na sasa vituo hivyo vinavyojulikana kama *Diplomatic Units* vinafanya kazi katika maeneo yanayopokea watalii wengi ya Arusha, Zanzibar, Tanga na Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa mkurugenzi mtendaji mkuu wa Tato, Sirili Akko, kutekelezwa kwa hitaji hilo la msingi ni mojawapo ya mambo makubwa yaliyofanywa na Serikali iliyopita huku mengine yakisubiriwa na wadau.

“Kwa sasa tuna mawasiliano na mahusiano mazuri sana na polisi maana vituo hivi vinatusaidia kutoa huduma maalum za watalii,” anasema Akko na kuikumbusha Serikali kukamilisha ahadi nyingine zilizotolewa na awamu iliyopita.

Anasema vituo hivyo hushughulikia changamoto maalum za watalii kama vile kupoteza stakabadhi au pasi za kusafiria na kuhitaji kufidiwa na mashirika ya ndege kutokana na kucheleweshwa safari zao.

Anasema usalama ni jambo muhimu kuongeza idadi ya watalii wanaoingia katika nchi yoyote duniani, inapotokea hali ya hatari katika nchi za jirani kwa kuwaepusha watalii kutembelea nchi hizo.

“Nakumbuka lilipotokea janga la Ebola katika nchi za Afrika Magharibi, lakini nchi zetu za Afrika Mashariki nazo ziliathirika. Usalama ni jambo nyeti sana kwa watalii,” anasema na kuongeza kuwa:

“Kwa sasa Tanzania haina jambo lolote kubwa la kiusalama japokuwa tunaathiriwa na kile kinachotokea nchi za jirani za Burundi na tishio la Alshabab Kenya. Na hapa ningeshauri nchi zetu za Afrika Mashariki kubadili sera zao za mambo ya nje na kufanya usalama kama jambo la pamoja kwa ukanda huu.”

**Changamoto za utalii nchini**

Utalii ni sekta muhimu kwa uchumi wa Tanzania. Kwa sasa ndiyo sekta inayoongoza katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni. Katika mwaka ulioishia Oktoba 2015, utalii ulizalisha Dola2.2 bilioza Marekani ni ikifuatiwa na dhahabu na viwanda ambavyo kila kimoja kilizalisha Dola1.3 bilioni za Marekani kwa mwaka huo.

Kupitia dira ya maendeleo ya 2025, Tanzania inatarajia kuzalisha Dola16 bilioni za Marekani kwa mwaka kutokana na sekta ya utalii. Kiwango hicho cha fedha ni kikubwa kuliko Bajeti ya Tanzania kwa mwaka 2015/16.

Pamoja na umuhimu huo, sekta ya utalii bado inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo wafanyabiashara wanasema zinahitaji kurekebishwa haraka.

“Tunaikumbusha Serikali kuongeza kasi ya ushughulikiaji wa kero za utalii ikiwamo ahadi ya kuunda chombo maalum cha kushughulikia changamoto zinazoikabili sekta ya utalii (Tourism lab). Tuna imani kubwa utekelezaji utakamilika hivi karibuni,” anasema Akko.

Mbali na ukweli kwamba Tanzania ni nchi ghali kwa watalii kuingia ikilinganishwa na nchi nyingine duniani, bado pia wafanya biashara wanalalamikia mazingira yasiyo rafiki kwao na utitiri wa kodi.

Akko anatoa mfano kwamba mfanyabiashara mmoja (Tour Operator) anatakiwa kulipa kodi tofauti zipatazo 32 tena zinazotozwa na vitengo tofauti na vingine vikiwa maeneo ya mbali kabisa.

Kwao, shida siyo kodi kubwa tu bali pia muda na rasilimali nyingine zinazotumika kufuata kodi hizo kwani wafanyabiashara hutumia siku 128 katika mwaka kwa ajili ya kulipa kodi hizo.

Tanzania inapokea watalii wapatao 1,000,000 kwa mwaka na kuajiri watu takriban 500,000, kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia (WB) kuhusu hali ya uchumi nchini iliyotolewa Januari mwaka jana.

Taarifa hiyo ilisema kwamba hata matarajio ya kupata Sh16 bilioni kutokana na utalii yanaweza kufikiwa iwapo kutakuwapo mabadiliko ya kisera na hata fikra za wadau wa sekta hiyo.

WB ilipendekeza namna tatu za kuboresha utalii wa Tanzania ili kufikia malengo na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi.

Kwanza, inapendekeza kupanua wigo wa shughuli za utalii badala ya kung’ang’ania ukanda wa kaskazini wa Arusha na Zanzibar tu ambao huchukua takriban asilimia 90 huku vivutio vingine vikisahaulika au kuharibika katika maeneo ya kusini, kati na magharibi.

Pili, anashauri kushirikisha jamii zilizopo kanda za kitalii na wafanyabiashara wadogo katika biashara pana ya utalii ili kuwanufaisha Watanzania wengi zaidi.

Tatu, Benki hiyo ilipendekeza kwa Serikali kurahisisha mifumo ya ulipaji kodi na kuhakikisha kuwapo uwazi katika mapato yatokanayo na utalii. Hali hiyo itapunguza gharama za miamala ya kodi na kuhakikisha usawa kwa walipa kodi.

**DONDOO**

Changamoto za utalii nchini kwa mujibu wa Benki ya Dunia

- Malipo mengi ya watalii bado yanafanyika nje ya Tanzania
- Tanzania bado imeelekeza nguvu katika ukanda wa Kaskazini wa Arusha na Zanzibar tu na kusahau vivutio vya maeneo mengine
- Jamii za maeneo husika bado hazijaunganishwa kikamilifu katika biashara ya utalii maana wengi ni masikini
- Utalii umekuwa ukikua kwa kasi lakini ajira zako bado ni chache

**SAUTI ZA WATU**

**Pius Makundi**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatakiwa kutoa elimu ya kutosha kwa mlipa kodi kabla ya yote. Watanzania wengi ni wasikivu ila hawajatengenezewa mazingira mazuri ya ulipaji kodi na kupewa elimu ya kutosha ili ifike wakati wawe na hamasa ya kulipa kodi wenyewe pasipo kushurutishwa na mamlaka yoyote. Ujio wa mashine za EFDs ulikuwa ni wa ghafla na mfanyabiashara hakuandaliwa kisaikolojia kupokea utaratibu mpya. Pia , gharama za mashine zilikuwa kubwa sana na wakati huohuo serikali haikupenda kusikiliza maoni ya walengwa. Sasa Serikali na mamlaka zake ni vyema wawe wanafanya tafiti kwanza kabla ya kufanya jambo kama hili la EFDs, kwa kuwa umakini ulikuwa mdogo na ndiyo chanzo cha kuibuka mgogoro mkubwa na wafanyabiashara ambao ungeweza kuepukwa kabla.

**George Mhema, Makamu Mwenyekiti TCCIA Mufindi**

Ni vyema Serikali iondokane na mifumo ya kuwabana wakulima juu ya soko huria kupitia vyama vya ushirika, maana maandalizi ya shamba, ununuzi wa mbegu, mbolea, palizi, dawa, mavuno hadi usafiri ni gharama za mkulima kwenda sokoni, hivyo anayejua gharama halisi ni yeye, kwa nini Serikali ipange bei? Kuhusu lumbesa Serikali na wadau wa biashara na kilimo kama TCCIA watoe elimu kwa wakulima juu ya hasara anayoipata mkulima na Serikali kwa kila gunia moja la lumbesa.

***Kwa maoni kuhusu mazingira ya kibiashara Tanzania, tuma ujumbe kwenda 0786240172. Ujumbe utakaochapishwa utazawadiwa Sh30,000 za muda wa maongezi.***

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA

BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo